# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**KENYA HIGH SCHOOL SCHOOL**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# KENYA HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/3**
**Karatasi ya 3**
**Mwongozo wa kusahihisha**

1. **a)Haki zinazomstahiki mtoto**

- makazi mema
- Usawa wa kijinsia
- Malazi mema
- Matibabu
- Elimu bora (zozote 4 x 1= 4)

**b) Mbinu za kishairi zinazotumika kutosheleza mahitaji ya kiarudhi**

i) Mazida - kutosheleza idadi ya mizani mfano: Mungavunja - mngavunja
ii) tabdila: kuleta mahadhi katika ushairi
mfano: Muhimidi - mhimidi
yamuepuke - yamwepuke
iii) Inkisari: Kutosheleza idadi ya mizani
kwa mfano 'Sidhurike - Usidhurike
Sinipe - Usinipe
hakiye - haki yake
iv) Kufinyanga sarufi / kuboronga sarufi - ili kuleta urari wa vina. Kwa mfano
i) Mpeni yaliyo yake - Yaliyo yake mpeni
ii) Kwa makini mumshike - Mmshike kwa makini
iii) Penye daraja avuke - Avuke penye daraja
Tan. Mwanafunzi lazima aeleze mahitaji ya kiarudhi (zozote 2 x 2 = 4)

**c) Umuhimu wa tamathali**

i) Istiari - i) Kuta nne zizunguke
ii) Penye daraja avuke
iii) Mpe taaluma yake
ii) Uhuishi i) Husuda mbi zimwondoke
ii) Apanuke bongo lake
iii) Maovu yamwepuke
iii) Taswira i) Apanuke bongo lake
ii) Titi alishike anyone (zozote 2 x 2 = 4)

d) Lugha nathari ubeti wa tano
Mtoto atibiwe ili asiathiriwe na magonjwa ili akue vizuri pia aweze kutambua rika lake na aelekezwe katika utu uzima. Haki za mtoto zisikiukwe (alama 4)

e) Toni - ushauri; kuelekeza (alama 2)

f) Maana ya msamiati
   i) mtima - moyo
   ii) Asihimike - asiteseke
   iii) mbi - mbaya/mbovu
   iv) Asighurike – asiangamie (ala ½ x 4 = 2)

**2.“Mtu huvuna alichopanda”**

a)

- Msemaji ni diwani wa watu
- Msemewa daktari Siki
- Nyumbani kwa Diwani wa tatu
- siki amemtembelea Diwani wa tatu kumshikinikiza aongee na Meya katika vikao vyao kuhusu matatizo yanayowakumba wafanya kazi (alama 4)

b) Wanaorejelewa walikuwa wamepanda pojo kwa sababu

- Walimchagua viongozi wandanganyifu Kwa mfano: Meya anadanganya kuwa dawa zimeagizwa ilhali ni uwongo

Wanawachagua viongozi fisadi
mfano: Meya ananyakua vipande vinane vya ardhi na kumgawia Bili vinne.

- Wanawachagua viongozi wanaopeana kandarasi kwa njia isiyo halali
- Viongozi waliochaguliwa kama vile Meya, Diwani I na II wanashirikiana kuuza fumbo ya Meya iliyo kitambulisho cha Umeya
- Wafanya kazi waliogoma wakidai haki zao za:
- Nyongeza ya mishara, gharama ya vitu kupanda, ukosefu wa dawa n.k, wanafurushwa vibaya na askari kwa amri ya Meya.
- Meya kama kiongozi aliyechaguliwa anakataa kushughulikia malamishi ya wafanya kazi. kama Nyongeza ya miashahara, kuletea wafanya kazi vifaa vya kufanyia kazi kama glavu za kuoshea choo. (Zozote 5 x 2= 10)

c) Sifa za mnenewa (siki)

- Mtetezi wa haki
- Ni mwajibikaji

- Ni mwenye busara
- Ni mshauri mzuri
- Ni mvumilivu
- Ni mshawishi
- Ni mwenye utu

Tan. Mwanafunzi lazima afafanue hoja zake

Kutaja alama $^1/_2$

Maelezo alama ½ (zozote 6 X 1= 6)

**3.**

- Matumizi mabaya ya askari tawala ambao wanawapiga watu risasi na kuwatupia vitoa machozi.
- Matumizi mabaya ya hazina ya baraza - Hazina inakuwa na nakisi.
- Wawakilishi wa wafanyi kazi kunyimwa nafasi ya kuongea na Meya.
- Ufisadi km. Meya kujilimbikizia vipande vinane vya ardhi na kumgawia Bili vinne.
- Matumizi mabaya ya mamlaka
- mfano. Mayors act na riots act.
- Wafanya kazi kutelekezwa katika utendaji kazi wao. Mfano: hawapewi glavu za kuoshea vyoo.
- Wafanya kazi kunyanyaswa.
- mfano wanalipwa mishahara nusu, Mshahara inacheleweshwa na wakati mwingine hawalipwi. Aidha hawaongezewi mishahara.
- Ukabila na mapendeleo- Meya anampigania mhazili ndio awezo kupata kazi
- Raia kuuliwa ovyo hasa wakati wa maandamano.
- Raia kutelekezwa kwenya njaa na magonjwa na kujifia kama nzi.

- Wanaotetea haki za wafanya kazi wanatengwa

  mfano: Diwani III na siki.

- Walio mamlakani kujiongezea mishahara
  mfano: Meya, Diwani I na II (zozote 10 x 2 = 20)

**4. a)**

-Maelezo ya mwandishi akimrejelea Bi Zuhura- Mkewe Mtemi Nasaba Bora
-Akiwa chumbani mwake ambako amejilaza kitandani
-Bi zuhura alikuwa na ukiwa kwa kuwa mumewe alikuwa amezoea kurejea usiku sana na kumpuliza kimapenzi

**b) i) Sifa za mrejelewa (Nasaba Bora)**

-Ni laghai
-Ni kiongozi fisadi
-Ni mwenye tamaa
-Ni mnafiki
-Ana taasubi ya kiume.
-Si mwajibikaji.
-Ni mwongo
-Ni mwaherati.
Tan. Mwanafunzi aeleze hoja zake kikamilifu
Kutaja $^1/_2$
Maelezo ½ ( zozote 5 x 1= 5)

**ii) Umuhimu wa Nasaba Bora**

- Ni kielelezo cha viongozi wa kiafrika wanaouendeleza ukoloni mambo leo.

- Awakilisha wanaume wenye taasubi ya kiume.

- Ni kielelezo cha viongozi katili katika jamii.

- Anawakilisha wanaume wanaosambaratisha ndoa zao kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa.

- Ni kielelezo cha viongozi wenye tamaa wanaojilimbikizia mali ya wanyonge.

- Anawakilisha viongozi laghai katika jamii.

Tan. Mwanafunzi aeleze hoja zake kikamilifu.
Kutaja ½
maelezo ½ ( zozote 5 X 1 = 5)

**c) Maudhui yanayodokezwa na dondoo**

**i) Upweke**

- Mumewe aliporejea nyumbani alijibwaga kitandani kama gogo la mti
- Anakumbwa na kiu ya njaa ya kimapenzi ya mumewe
- Wanawake wengine walishinda na kukesha pamoja na wanaume zao
- Alikuwa na umaskini wa kimapenzi licha ya kuwa na mali chungu nzima
- Alikosa kustahiwa na mumewe

**ii) Ndoa**

- Asasi ya ndoa imejaa mateso dhidi ya mwanamke
- Wanaume hawakuiheshimu asasi ya ndoa. mfano Nasaba Bora ana uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa
- Wanawake wanakumbwa na upweke mfano; Bi Zuhura ametelekezwa kimapenzi.
- Wanawake wanaachiwa mzigo wa malezi km. Dora

**iii) Ukatili**

- Bwana Nasaba Bora anamshuku mkewe kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Amani.
- Wanawake hawashauriwi.

mfano: Majisifu anakataa kumshauri mkewe kuhusu uamuzi wa kumleta Amani kwao.

**iv) Umaskini**

- Kuna wanawake waliovalia rinda moja siku baada ya nyingine.
- Wanasokomoko wengi walikuwa wahitaji.
- Watoto waliajiriwa kuchunga ng'ombe na hivyo kukatishiwa masomo yao. (Maudhui yoyote 3 X 2 = 6)

**5. Mla naye huliwa zamu yake ifikapo**

- Nasaba Bora anatoza wanasokomoko pesa ndio Madhubuti aende ng'ambo, madhubuti anaporudi nyumbani kutoka ng'ambo, anamuasi baabake.

- Nasaba bora anawatuma askari kumvamia na kumuua mamake Imani, baadaye yeye (Nasaba Bora) anavamiwa na genge la Oscar kambona na nusura auliwe.

- Nasaba Bora anamwachisha Lowela masomo kutokana na uhusiano wa ki-mapenzi naye, baadaye Mashaka anakatiza masomo yake kwa kuathirika na barua ya Ben Bella ya kukata uhusiano wao wa kimapenzi.

- Nasaba Bora anawatia gerezani Amani na Imani kwa tuhuma za kuua, hata hivyo ng'ombe wake wanaroroma kwa uchungu kwani hawakuwa wamekamuliwa. Aidha, inamlazimu Bi. Zuhura, kumwandalia mwalimu majisifu chai ya mkandaa.

- Nasaba bora anahonga wakubwa jeshini ili kumtafutia Madhubuti kazi; hatimaye, pesa zile zinapotea madhubuti anaporudi kutoka ulaya na kuikataa kazi hiyo; na kutaka kujitafutia nyingine kwa jasho lake.

- D.J analihurumia jimwa jimmy ambalo lilikuwa limefungwa kwa minyororo na kumshauri Bi Zuhura liachwe huru. Mwishowe linapokata minyororo na kuwa huru, linamng'ata Dj mguuni vibaya sana.

- Chechwe makweche analimbikiziwa sifa nyingi kwa kuwa mwana soka hodari nchini Tomoko, hata hivyo anawasahau nduguze na mamake. Aidha anapovunjika fupaja serikali inamtekeleza na pia anakosa ndugu wa karibu wa kumsaidia

- viii)Mwalimu majisifu anadhani ni siri yake mwenyewe kuhusiana na wizi wa mswada na Amani, hatimaye anagundulika na Amani mwenyewe wakati anapomtuma Imani kumwombea vitabu vya kusoma kutoka kwa mwalimu majisifu.

- Mwalimu Majisifu anamkashifu Mashaka kwa kutosoma kitabu cha kidagaa na hata kusema hastahili kuitwa mpwa wake, aidha anapoenda kutoa mhadhara katika chuo cha mkokotoni anashindwa kujibu maswali kuhusiana na kitabu chenyewe.

- Nasaba Bora anawatesa na kuwauwa watu ili anyakue mashamba yao, baadaye anapomfunulia ukweli Amani kuhusiana na hayo mashamba anatowekea msituni na kujitia kitanzi.
  (zozote 10x 2 = 20)

**6. <u>Ubaguzi</u>**

**a. Mke wangu**

- Mwanamke anachukuliwa kama ndiye anafaa kuongozwa na mwanamume.
- Wachumba wanapotaka wake, waliosoma wanabaguliwa
- Watu wa daraja la chini hukaa mashambani nao waliosoma wanaishi mjini.
- Wenye vyeo vya juu hawatangamani na wale wa vyeo vya chini.

**b. Samaki wa nchi joto**

- Sehemu za starehe zilitengewa wazungu kwani wale weusi hawangeweza ada zilizotozwa za juu.
- Wanaoishi katika mitaa bora uliyokuwa na huduma bora ni wazungu, 'ilihali, wale hawakuwa nacho wanaishi katika mitaa duni.
- Waliokuwa wa tabaka la juu walikuwa na watumishi.

**c. Damu Nyeusi**

- Fikirini alilikuwa akiulizwa maswali ya kuumbua na wazungu.
- Wahadhiri waliwanyima Waafrika alama katika mtihani ingawa walistahili.
- Dereva wa gari anakosa kulisimamisha gari kumchukua Fikirini.
- Waafrika wanapoenda kununua bidhaa katika maduka makubwa wanafuatwa na walinzi wakidhaniwa kuwa wezi.

**d. Kikaza**

- Viongozi wanakula vizuri huku wananchi wakikosa chakula
- Viongozi wanawabagua wananchi na wanakuwa walafi
- mfano wa kobe.
- Wanawake hawapewi nafasi ya kuongoza.

**e. Maeko**

- Jamila anapigwa na kutukanwa mara kwa mara.
- Duni anabaguliwa na kulengwa na jamii kwa ulevi wake.
- Jamila anabaguliwa kimapenzi na mumewe.

**f. Kanda la usufi**

- Mwanamke anabaguliwa kwa kupewa jukumu la ulezi ilhali ulezi ni wa mume na mke
- Sera anabaguliwa shuleni kwa sababu ya mimba.
- Sera alipofukuzwa shuleni, Masazu hakuathirika

**g. Maskini babu yangu**

- Wenye mali wanaishi katika mitaa bora, uhali maskini wanaishi katika mitaa duni
- Ubaguzi wa kikabila katika ndoa (zozote 5 x 4 = 20)

**7. a)**

- Haya ni maelezo ya mwandishi
- anawarejea Chris Masazu na wanafunzi wengine wa kiume waliozuru kila sehemu ya shule ya upili ya Askofu Timotheo na kutaka kuacha kumbukumbu ya ziara yao katika shule hii kwa kuwatafuta wanafunzi wa kike ili wawe wapenzi wao (alama 4)

**b) Michezo ya ujana**

- Wengi wanajiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na kuringwa kama, sela.
- Sela anakatiziwa masomo yake ili aitunze mimba yake.
- Vijana hujiingiza katika ndoa za mapema.
- Kutomakinika masomoni kama Masazu na Sela.

- Watoto wanaozaliwa kutopewa malezi mema (zozote 4x 2 = 8)

c) **Tamaa mbele mauti nyuma**

- Lucy anatamani sana maisha ya London japo hakupata gredi ambayo ingemwezesha kuishi huko.
- Lucy anatamaa ya kufika ulaya hivyo anaamua kuolewa na mzee Crusoe ambaye hakumpenda.
- Lucy ana umri mdogo na anaamua kuolewa na mzee mkongwe, dhaifu na asiye na nguvu za aina yoyote.
- Lucy anaingiwa na upweke na anamchukia mzee Crusoe ila anajifanya anampenda akingoja kifo cha haraka cha mzee Crusoe ili ajitajirishe na pesa zake.
- Alitaka amrithi mzee haraka, hiyo haraka ikimzamisha katika mauti yake. (Zozote 4 x 2 = 8)

**8. a) Sifa za ushauri simulizi**

- Kuna msimulizi na hadhira.
- Huwa na mpangilio wa beti au fungu.
- Huwa na lugha ya mkato.
- Huelezea hisia za ndani za msemaji.
- Hutegemea sauti na toni.
- Huweza kutambulishwa na ala za muziki.
- Viziada lugha hutumika km. ishara za uso.
- Huweza kutungwa papo hapo km. sifo.
- Huelezea tukio maalum la kihistoria.
- Huhusisha utendaji jukwaani. (zozote 4 x 2 = 8)

**b)** Aina tatu za maigizo.

- Michezo ya jukwaani.
- Majigambo.
- Vichekesho.
- Ngojera.
- Michezo ya watoto.
- Miviga.
- Ngomezi.

Tan: Mwanafunzi lazima aeleze hoja zake kikamilifu
kutaja 1 maelezo 1 (zozote 3 x 2 = 6)

**c)** Mbinu za kimtindo za methali

i) taswira/ picha za akilini
Mfano - paka akiondoka panya anatawala.
- Mtupa jongoo hutupa na mtiwe.

ii) Urudiaji/ takriri
Mfano: - Haba na haba hujaza kibaba
- Bandu bandu huisha gogo

iii) Vichezea maneno / mchezo wa maneno
Mfano: i) gunia nzima angerudi na upele
ii)Mkele haendi ukele na angeenda ukele na kujaza mlele

iv) Tanakali za sauti - Chururu si ndo! ndo! ndo!
- Kiliacho pa! kijutie

v) Mbinu za kishairi kwa mfano: Vipande na mizani
- Haba na haba, hujaza kibaba
- Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi
hoja – ½ mfanon ½ (Zozote 4 x 1 = 4)

d) Umuhimu wa hekaya.
-Huonya juu ya upumbavu.
-Hutoa maadili kwa wanajamii ili waache kuwatendea wenzao ujanja.
-Huwaokoa wanaodhulumiwa kwa kutumia uwezo mkubwa wa akili walionao.
-Hufunza watu kutenda mema.
-Hufunza kutokana na ulimwengu uliojaa hila na shaka, wema na uadilifu.
(zozote 2 x 1 = 2)